

KUMZALIA MUNGU MATUNDA

Warumi 7:1– 6” Ndugu zangu, hamjui (Maana nasema na hao waijuao sheria), ya kuwa torati humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai? Kwa maana mwanamke aliyekuwa na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai, bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume. Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapo olewa na mume mwingine. Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda. Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata tukaizalia mauti mazao. Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani ya andiko”.

Hebu tusikilize kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo:-

Siku zote, usipime maisha yako kwa nguvu ulizo nazo za kufanya miujiza. Na hatujipimi wenyewe kwa kiasi cha maarifa ya Neno tuliyo nayo. Lakini siku zote tujipime wenyewe... Angalia nyuma na uchunguze ni aina gani ya tunda la maisha unayozaa kwa sasa. Unaona? Kama nilivyohubiri wakati uliopita juu ya kumdhihirisha Yesu kudhihirisha maisha ya Kikristo [1]

Mwombe Mungu kuifanya Nuru ya siku hii ya leo iangaze ndani yako ikufanye uwe mtumwa mtiifu kwa Mungu, na uache tunda la Roho lidumu katika maisha yako. Na hayo ni maisha yanayoistahili Injili.

Njia pekee uwezayo kuishi maisha yanayoistahili Injili ni kuiacha Injili yenyewe, kila kitu cha Injili, kije ndani yako na kidhihirishe ahadi zake alizoahidi, kuzifanya zidhihirike. Mwache Mungu aishi ndani yako kuthibitisha ahadi za siku ya leo.

Kama vile Yesu alivyomwambia Yohana” kubali hivi sasa, Yohana hiyo ni kweli, sisi ni wajumbe wa siku hii ya leo, na imetupasa kutimiza haki yote” (Matayo 3:13-17).

Na kama tu wakristo wa siku hii ya leo, na tumpokee Yesu Kristo ndani ya mioyo yetu. Na Yeye ni neno. Usikatae lolote. Sema, “Hiyo ni kweli” na liweke moyoni mwako, na uangalie tunda la Roho juu yako, na timiza kila ahadi aliyoahidi katika Biblia. Mungu anataka kutimiza Neno lake, na hana mikono

ila yangu na yako. Hana macho yoyote ila yangu na yako. Yeye hana ulimi ila wako na wangu. “Mimi ni mzabibu; nanyi ni matawi” (Yohana 15:1-7) Matawi ndiyo yanayozaa matunda. Mzabibu unatia nguvu matawi. Hayo ni maisha yanayostahili [2].

Tunda la Roho leo ni upendo, furaha, Imani, uvumilivu, upole, utu wema, subira, na vyote ni vya kimiujiza [3]. (Galatia 5:22-23).

Amebarikiwa mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji, wala hakuketi barazani pa wenye mizaha... (Zaburi 1).

Atazaa matunda yake kwa majira yake (mwanzo 1:11), Atazaa matunda yake. Matunda gani? Tunda la nini? Tunda lake. Tunda gani? Tunda lake mwenyewe. Hilo ni tunda gani? Ni Biblia. Unaona? Vyote viko hapa, lile tunda: upendo...uko hapa katika Biblia. Furaha...iko hapa kwenye Biblia; nguvu; Roho mtakatifu; mambo yote hapa; uponyaji wa Kiungu; ahadi za Mungu. Hayo ndiyo matunda. Hili hapa, na kama amepandwa katika hili, hili limepandwa katika udongo mzuri, katika Imani. Imani inafanya nini? Imani inaanza kulikuza Amina. Inaanza kumwinua juu. Unaona? Hilo hapo: Linainuka juu. Hakika! Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uzao matunda kwa majira yake.

Sasa, ni tunda la aina gani atakalozaa? Yohana 14:12 Yesu alisema, Yeye aniaminiye mimi kazi nizifanyazo Yeye naye atazifanya ... kwa nini? Neno lile lile ndani yake. Yeye alikuwa Neno. Hiyo ni sawa? Na Kama mkikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu, ombeni mtakalo (Mt. Yohana 15:7).

Mito. Ni nini? Karama zile tisa (Ikor 12: ... mito ya aina moja ya maji, Roho mmoja... maji aina moja, lakini yakitoka katika vyanzo tofauti tisa. Mito ya maji, unaona, mito ya maji... Hilo huzaa tunda lake... (Tunda la Roho) katika majira yake; wala jani lake halinyauki; na kila alifanyalo litafanikiwa (Zaburi 1:3) [4].

Mzabibu wa kweli na mzabibu wa uongo yote inao upako wa aina moja. Maji yakiinyesha yote (Matayo 5:43-45). Sio ajabu alituonya sisi kwamba itadanganya hata aliyemteule kama ingewezekana (Matayo 24:24).

Angalia. Ilionekana yote inafanana; imepakwa upako yote. Lakini angalia, kwa matunda yao... (Matayo 7:15-20) utajuaje kuwa haya sio machungwa? Kwa sababu unazaa zabibu. Ule mzabibu uko sahihi; unaishi ndani ya huo mti; lakini unazaa zabibu. Hauko kama ule wa kwanza. Na kama Kanisa linasema linamwamini Yesu Kristo yule yule, jana na hata milele, na linakana nguvu zake, linakana kazi zake, linakana Neno lake... Kanisa ambalo linamwamini Yesu Kristo litafanya kazi za Yesu Kristo; litakuwa na uhai wa Yesu kristo. Na kama

haliko hivyo... Haijalishi hata kama uhai unamwagwa juu yake, kama halikuteuliwa kimbele kutoka kwenye mizizi, litazaa zabibu. kila mara au kitu kingine tofauti. Lakini kama ni uhai uliochaguliwa kimbele kutoka mizizini, litazaa Yesu kristo yule jana, leo, na hata milele, kama Neno linakuja kutoka mizizini, ambaye ni shina, mwanzo wa wakati.

Angalia, ni kile wanachozaa ndicho kinaonyesha tofauti: kwa matunda yao” Yesu alisema, “Mtawajua” mtu hakusanyi zabibu kutoka kwenye miiba hata kama hiyo miiba iwe ndani ya mti wa mzabibu. Hilo linawezekana, lakini matunda yatakueleza. Tunda ni nini? Lile neno, La... tunda la wakati, hilo ndilo hasa, mafundisho yao. Mafundisho ya nini? Mafundisho ya wakati, ni wakati gani huu... mafundisho ya watu, mafundisho ya kidhehebu, au Neno la Mungu la wakati.

Balaamu, akiwa amepakwa mafuta na Roho yule yule aliyekuwa na Musa... tofauti ilikuwa ni nini?

Mafundisho ya Musa yalikuwa (sahihi) makamilifu. Biblia ilisema hapo katika 2Petro kwamba ilikuwa ni mafundisho ya Balaamu ambayo waisraeli waliyapokea na Mungu kamwe hakuwasamehe. Dhambi isiyosameheka (Hesabu 25:1-5). Hakuna hata mmoja wao aliyeokolewa. Ingawa walikuja chini ya baraka za Mungu na kuuona mkono wa Mungu ukitenda kazi kwa Nabii huyu mkuu nak uona kabisa ikithibitishwa na Mungu, na kwa sababu nabii mwingine alikuja na mafundisho yaliyo kinyume, na kubishana na Musa, na kujaribu kuwathibishia watu kwamba Musa amekosea... (Hesabu 16:1-35) na Dathan, Korah, na wengi wao walikubaliana naye na kuwafundisha wana wa Israeli wafanye uasherati, kwenda kwenye dhehebu lake na kusema sisi tuko sawa, “Kama tu Methodist, Baptisti, Presbyterian au Pentecoste na mengineyo, sisi wote ni sawa.” Ninyi ni watu mliotengwa, watakatifu kwa Bwana, waliowekwa wakfu kwa Neno na Roho wa Mungu kuzaa matunda ya ahadi ya siku ya leo. Na wewe sio sawa na wao.

Sasa, mafundisho ya Balaamu.. siyo unabii wa Balaamu, huo ulikuwa ni sawa; huo ulikuwa ni Mungu. Wangapi wanaamini hilo? Unabii wa Balaamu ulikuwa sawa sawa kabisa, kwa sababu asingeweza kuzungumza chochote. Upako ule wa Mungu usingeweza kuzungumza kitu cha tofauti. Na Mungu alikithibitisha na kukihakikisha kwamba ilikuwa kweli. lakini ilikuwa ni mafundisho ya Balaamu. Sasa linganisha hilo na Matayo 24:24. wapakwa mafuta, lakini mafundisho yao ni uongo, ule utatu na mambo mengineyo kama hayo siyo sawa, upinga Kristo [5].

Ndipo Yesu alipokuja. Siku ile Yesu aliyokuja, watu wale walilijua Neno la Mungu kama andiko tu. Si ndiyo? Hakika, lakini walikuwa wajinga juu ya Yeye alikuwa ni nani, walipomuona Mungu katika mbawa za hua (Mt. Yohana 1:29-34), akitenda na kufanya vile hasa alivyosema kuwa atafanya. Na alipofanya vile

hasa Neno lilisema. “Kama sizifanyi kazi za Baba yangu, basi na msiniamini mimi” Lakini Yeye alifanya vile ambavyo Neno lilisema

atafanya. Na walikuwa ni wanasayansi katika siku hizo, lakini wajinga wa kisayansi kutenda dhambi ya makusudi.

Tamaa iliwapofusha. Wanahitaji Neno la Mungu kumuonyesha yu uchi. Ufunuo 3 ilisema “ Nakupa shauri ununue kwangu, dawa, kwamba macho yako yafunguliwe, na kwamba uweze kuiona aibu ya uchi wako (Ufunuo 3:18).

Dawa ni Neno la Mungu, uponyaji wa macho unaokutoa kutoka kwenye mambo ya asili ya ulimwengu, na kukubadilisha kwa nguvu za Mungu kukuleta uweponi pake. Hapo sasa unaona. Unasema, “ nilikuwa nimepotoea, sasa nimeonekana. Nilikuwa kipofu, lakini sasa naona” Unaona? Itakuwa tofauti. Huo ndio mwito wa Kanisa leo, ni “ nakupa shauri uje ununue kwangu dawa ya macho yako, ili uwe aliye na upako wa dawa yangu, na hapo utaona”.

Mwache Roho Mtakatifu aje juu ya mtu yoyote ambaye kwa kweli anakitu pale ndani... uponyaji unakuja kutoka ndani. Acha uponyaji uje kutoka kwa Roho Mtakatifu aliye ndani yako. Kama ni Roho halisi anayeipaka mafuta mbegu halisi haiwezi ikafanya chochote ila kuzaa matunda, mwana au binti wa Mungu. “ Lakini Roho halisi ya kweli inaweza ikaja juu ya mbegu ya gugu; mvua inaweza ikanyesha juu ya gugu, na italifanya liishi sawa kama inakuja juu ya ngano na kuifanya iishi. “Lakini kwa matunda yao utawajua” unaona? Sisi ni mti wa matunda wa Mungu, tukizaa Neno lake [6].

Waangalie Wapentekoste walivyolipapatikia hilo miaka iliyopita “Na sisi, Kanisa... Sisi, Kanisa” ni mwili wa Kristo. Ni mtu Binafsi miongoni mwa watu binafsi ambao wamezaliwa katika ufalme wa Mungu. Hilo linatoka kutoka ndani kuja nje. Unaliishi tu kirahisi.

Humuambii kondoo azae manyoya au atengeneze manyoya, Ninamaanisha. Kondoo hahitaji kutengeneza manyoya. Sema sasa Bwana wangu ananitaka niwe na manyoya mwaka huu. Inabidi mranye bidii. Hapana, jambo moja analopaswa kufanya nikubakia kondoo. Hiyo ni sawa. Sufu itatokea tu, kuzaliwa....

Na hatuambiwi tutengeneze matunda; tunapaswa kuzaa matunda kuwa na matunda; unaona? Tunapaswa kuzaa matunda. Na ili mradi wewe ni mti wa matunda wa Mungu pamoja na Neno la Mungu, Neno la Mungu litajithibitisha lenyewe. Litazaa matunda ili mradi Neno liko pale na Yesu alisema, “ Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lolote nanyi mtatendewa” (Mt. Yohana 15:7) unalionga hilo? Hutengenezi kitu.

Hujaribu kuiamsha nia kwa hilo; Ni Kwamba liko pale tu. Na linaendelea na kuendelea na kuendelea.

Sasa wengine wanaendelea mbali hata kuwa wazushi. Sasa wanaenda upande wa pili. Na wanafikiri ili mradi wanaruka juu na chini au wanapata namna ya muwasho au msisimko, kunena kwa lugha, au kutoa unabii ambao umetokea kuwa kweli au kitu fulani kama hicho, wanafikiri ndicho chenyewe. Wamekipata lakini sio hivyo.

Yesu alisema.” Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kufanya kazi nyingi nakutoa pepo? “Atasema ondokeni kwangu, sikuwajua kamwe” (Matayo 7:21-23) Unaona? Hiyo siyo yenyewe. Hiyo sio yenyewe marafiki. Ndiyo sababu ishara ya lugha... Naamini katika kunena kwa lugha, lakini si chukulii kwamba ndio ushahidi pekee wa Roho Mtakatifu. Hapana Bwana. Tunda la Roho ndio ushahidi.

Unaona, hiyo ndiyo sababu ninatofautiana na madhehebu ya ndugu zangu Wapentekoste katika ile namna wasemavyo kuwa “Kama mtu akinena kwa lugha, ana Roho Mtakatifu”. Natofautiana nao. Hiyo siyo ishara ya kwamba ana Roho Mtakatifu. Unaona? Nimesikia mashetani yakinena kwa lugha kwa haraka kadri yalivyoweza, kunywa damu kutoka kwenye kichwa cha mtu na kuita mashetani.

Nimewaona wahindi wakichukua nyoka na kumfunga kuwazunguka wao wakati wa dansi za mvua kule nje Arizona, na kunyosha mikono yao juu kama hivyo, na kukimbia kuzunguka; na mganga wa kienyeji anatoka akijikatakata mwenyewe, na kuweka penseli chini, na inaandika kwa lugha isiyojulikana na kutoa tafsiri. Kwa hiyo, unaona? Usiniambie mimi hivyo. hapana, ni mtu mzima vyakutosha.

Tunda la Roho ndio (ushahidi) Yesu alisema, “kwa matunda yao (siyo kwa lugha au msisimko lakini) kwa matunda yao mtawatambua.” kwa hivo hilo ni tunda la Roho.

Ni Mungu akijifunua mwenyewe katika unyenyekevu, utamu, na kila siku ni hivyo. Ni kitu fulani juu ya mtu anayekaa hasa na Neno, kila mara akiliona Neno, huliitikia na “Amina,” Haijalishi watu wengine wanasemaje... Yeye analiamini hilo Unaona? [7].

Mpaka Mtu azaliwe mara ya pili (Yohana 3:1-8). Wakati amezaliwa tena, uhai wa Mungu unakaa ndani yake. Na hapo, sasa tunda la Roho linafuata, ambalo ni, upendo, Amani, furaha, uvumilivu, fadhili, upole, utu wema, subira. Anakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo Yesu (2Kor 5:17). Naye ni sehemu ya Mungu, mwana wa Mungu. Hawezi akafa kama vile Mungu asivyoweza kufa. Yesu alisema, “Yeye alisikiaye Neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna (sasa) uzima wa milele, na wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani.” (Yohana 5:24) [8].

pili, Mungu anakuthibitisha. Hivyo ndivyo Mungu anavyothibitisha vitu vyote vya asili. Kwa nini? Kwa matunda yao. Hivyo ndivyo anavyothibitisha huduma yake. Hiyo ni kweli. Watumishi wake wote wanathibitishwa hivyo hivyo anavyothibitisha vitu vya asili. Utajuaje ni mti wa peach? Kwa sababu unazaa mapichezi. Utajuaje ni mti wa mtofaa? Unazaa matofaa. Unajuaje ni Mkristo? Ishara za mkristo zinazaliwa kutoka kwake; maisha ya Kikristo yanatoka ndani yake. Unajuaje ni mwalimu? Neno linatoka kutoka kwake. Utajuaje yeye ni Nabii? Neno linakuja kupitia yeye. Linazaa matunda, linathibitishwa. Limejihakikisha lenyewe. Linakuwaje hivyo? Linapokufa na kuwa mmoja. Hiyo ni sahihi. Tunapokufa na kuwa viumbe vipya ndani ya Kristo Yesu, linatupata pamoja na mwito wetu; Tunakaa pamoja na wito wetu. Tunda la Roho linafuatana nasi kama sisi ni watumishi wake. Tunapozaliwa mara ya pili, matunda ya maisha ya Kristo yafuatana nasi. Hiyo ni sahihi. Unajuaje ni mti wa mpichi? Una mapichi. Unajuaje ni mkristo? Anatenda kama Kristo. Anatembea kama mkristo; anazungumza kama Kristo; anaishi kama Kristo; juu ya dhambi, mshindi; Anafanya nini? Unasema “Umeona nilivyofanya”? Kristo hakufanya hivyo. Alitoa utukufu wote kwa Baba. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo unavyojua hilo. Kwa matunda yao utawatambua. “Amini, Amini, nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa mbinguni.” (Mt. Yohana 3:3) [9].

Hakuna kitu katika Biblia kilichoachwa kama ushuhuda kwa Roho Mtakatifu, Ni tunda la Roho tu. Tafuta mahali popote ambapo Yesu alisema hivyo. Ndiyo Bwana. Ushahidi wa Roho Mtakatifu ni Tunda la Roho wako. Yesu alisema hivyo. “Utawajua kwa matunda yao.” Na tunda la Roho ni upendo, furaha, Amani, Uvumilivu, fadhili, amani, utu wema, upole. Na tunda la adui ni uadui, chuki, hasira, ugomvi, na kadhalika; hilo ni tunda la Adui. Kwa hiyo unaweza ukajipima kwa maisha unayoishi, umesimama wapi na Mungu. Kama moyo wako wote uko katika upendo Naye, na wewe unampenda na ni mtu mwema na unaishi naye kila siku, unajua umepita k 7 nautini kuingia uzimani. Kama siyo na uko vinginevyo, wewe unaigiza tu Ukristo. Hiyo ni sahihi. Ambapo waigizaji wote wa kimwili watawekwa wazi tunajua hilo.

Kwa hiyo usiishi maisha ya aina hiyo hupaswi kufanya hivyo kwanini ukubali kitu badala, wakati anga lote juu limejaa vitu vizuri na halisi? Hakika. Hebu nimchukue Mungu, hicho ndicho ninachohitaji. Amin. [10]

Na sasa angalia kama wakati ule wa kwanza, alipoanzisha lile Kanisa la kwanza ambalo kiwavi (tunutu) cha kiroma kilikula (na madumadu na kadhalika), alianza na kuhesabiwa haki kwa Imani. Katika Yohana Mtakatifu sura ya 17, mstari 17, Yesu alisema “Uwatakase Baba, kwa ile kweli. Neno lako ndiyo kweli.” Kazi ya pili ilikuwa ni utakaso (kwa Kanisa). Baada ya kuhesabiwa haki kwa Imani kunakuja utakaso. Na Baada ya kutakaswa, aliwaambia wangoje katika mji wa Yerusalemu Luka 24:49 mpaka wamepokea uwezo utakao juu, na pale ule mti ulizaliwa, yule Roho Mtakatifu, Pentekoste. Kuhesabiwa haki kwa imani,

kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na baadae Kristo akaja kukaa ndani yake kuufanya uzae matunda Amini. Hiyo ni sahihi? (Warumi 6:20 – 22) [11] Mafarisayo, Masadukayo, watu wakubwa, watu watakatifu, watu wazuri watu wema, watu wanyenyekevu, watu waliokuwa na tunda la Roho zaidi kuliko vile Yesu alivyoweza kuvitia katika mazoezi.

Lakini ni nini kilikuwa kitambulisho chake? Kwamba Neno lilikuwa pamoja naye, Neno lililoahidiwa la siku ile lilikuwa linaishi kupitia yeye. Alisema nani miongoni mweni anayeweza kunihukumia dhambi? Nani anayeweza kusema kile nilichodai hakikutokea? Kwa maana Yeye alionyesha kuwa ni mnadhiri wa Bwana aliyetengwa. Alikuwa ni Bwana mwenyewe katika mwili. [12]

Mmemuona kuhani wenu akionekana kama hivyo? Sasa tunda la Roho liko wapi? “Unaona?” Siyo kwa kunena kwa lugha, siyo kwa kucheza katika Roho, siyo kwa kujiunga na Kanisa, siyo kwa tunda la Roho (wakristo wa kisayansi wanamshinda yoyote kati yenu, unaona, na hata wanakanusha kwamba Yesu Kristo siyo Mungu). Siyo hiyo, bali ni Neno likiishi. Hilo pale. Kama tu wangeangalia. Alikuwa ni masihi. Alikuwa Neno lililohai lililofanyika mwili. Na mwanaume au mwanamke aliye na Roho wa Mungu ndani yake, lile Neno linaishi hasa ndani yao. Hicho ndicho kiini cha mdundo, wale waliochaguliwa kimbele. Kwakuwa Neno la Mungu linakuja kwao, na wao ni Neno kwa watu: Barua zilizoandikwa zisomwazo na watu wote (2Kor. 3:1 – 3). Hiyo ni sahihi? Inawezekana mvuto wa tatu umeshaanza? [13]

Tunda la Roho ni nini? Udhihirisho wa Neno lililoahidiwa. Kama tu wangesimama na kuangalia, Hakuwa na vitu vile walivyo kuwa navyo, Tunda la roho, au chochote. Lakini Neno lililoahidiwa la siku ile lilikuwa linajidhihirisha lenyewe, hiyo ilikuwa sawa kabisa Nuru ya saa ile hilo ndilo. Haijalishi ni Elimu kiasi gani, na ni karimu kiasi gani, umenena kwa lugha kiasi gani ni karimu kiasi gani, wema na kila kitu ulicho, labda tu ukubali lile Neno la saa ile linapodhihirishwa mbele zako, utakuwa kwenye hatari hiyo hiyo. [14]

Ninaomba, sasa, Baba, kwamba utawalinda kwa Neema yako mpaka siku ile kuu, ambayo inaweza ikawa kesho, kwamba itawapasa kusimama uweponi pa Mungu. Haijalishi wamefanya nini: wanaweza wakawa wakweli sana; wanaweza wakawa watiifu sana; wanaweza wakavaa vizuri sana, wakatenda vizuri sana, na kujiunga na kila Kanisa na bado wapotee. Hakuna cha Mkononi tunachokuletea. Hakuna tuwezacho kufanya kinachoweza kutustahilisha. Tunatumainia Neema yako. Na tunapofanya hivyo, ndipo maisha yetu yanabadilishwa na kuzaa matunda kwa Kristo. [15]

Nukuu za kiingereza:

- [1] Paulo mfungwa wa Yesu Kristo uk. 8 [2] Je maisha yako yana stahili Injili Aya 271 – 272. [3] Sauti zisizo na uhakika aya 39
- [4] Hekima dhidi ya Imani u. 16. [5] Wapakwa mafuta wa siku za mwisho. Aya 57 – 59, 67 – 71.
- [6] Nguvu ya kubadilishwa (65 – 1031M) Aya 272 – 276
- [7] Mungu katika urahisi uk. 38 – 39 [8] Simama kimya (57 – 0518) Aya 41. [9] Lazima uzaliwe upya Aya 187.
- [10] Waebrania sura 6 sehemu ya 2 Aya 495 – 496
- [11] Kurudishiwa mti ule wa Bibi arusi uk 68
- [12] Neno la Mungu linatuita kujitenga kabisa na kutokuamini Aya 66 – 67. [13] Nafsi zilizoko kifungoni sasa uk. 50 – 51
- [14] Kitendawili Aya 229 – 232.
- [15] Mkuu kuliko Sulemani yuko hapa (58 – 0625) Aya 56

Jiwe la kiroho la kujengea no. 147 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, D – 75328 Schomberg, Germany. simu (+49) 7235 -7613, Fax (+49) 7235 – 3306.

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya haraka itaizunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho Uk. 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,
Box 553 Korogwe - Tanga
E-mail: Chaelika@livel.com
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*